# SINGIDA SECONDARY SCHOOL
## SHULE YA SEKONDARI SINGIDA
**S.L.P. 589 – SINGIDA**
**SIMU NA: 0759-032918, 0784-716695 & 0679-446992**
**E-mail: singidasec@gmail.com**


**S. 1136**

Kumb. Na: ……………………………………….………
Tarehe: …………………………………………………..

Ndugu ……………………………………………………..
……………………………………………………..
…………………………………………...............
…………………………………………...............

**YAH: <u>MAELEZO YA AWALI KWA MWANAFUNZI ANAYEJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI SINGIDA</u>**

Ninayofuraha kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha ……………………….. katika shule ya Sekondari Singida.

Kwanza Shule inachukua nafasi hii kukupongeza na kukukaribisha, aidha tunaamini kwa wakati wote utakapokaa shuleni utazifanya kazi zako kwa juhudi, maarifa na uadilifu ili kuendeleza jina la Shule.

- Shule ya Sekondari Singida ni shule ya Bweni kwa wavulana na wasichana. Pia kutwa kwa wavulana na wasichana.
- Shule hii ipo upande wa Magharibi mwa Makao Makuu ya Mkoa wa Singida kama kilometa 5 kutoka katikati ya mji, kando ya barabara inayokwenda Kiomboi kupitia Ndago.
- Tunakufahamisha kuhusu vifaa vya muhimu na ambavyo ni lazima uje navyo siku unapokuja hapa shuleni. Bila ya vifaa hivi shule haitakupokea.
- Mwanafunzi hataruhusiwa kuendelea kidato kingine bila kufikia kiwango cha ufaulu ambao ni alama **45 (C).**
- Michango unayopaswa kutoa Mzazi/Mlezi ni sehemu ya kuchangia elimu kama ifuatavyo:-

**<u>O -Level</u>**

(a) Karo ya Bweni (Kwa Mwaka) Tshs. 1,500,000/=
(b) Karo ya Kutwa (Kwa Mwaka) Tshs. 900,000/=

**ADA ILIPWE KWA UTARATIBU UFUATAO:**

| **MUHULA WA KWANZA** | | |
|---|---|---|
| **MIEZI** | **BWENI** | **KUTWA** |
| **O - level** | | |
| January – April | 400,000/= | 250,000/= |
| April – June | 350,000/= | 200,000/= |
| **MUHULA WA PILI** | | |
| **O - level** | | |
| July - September | 400,000/= | 250,000/= |
| September - December | 350,000/= | 200,000/= |

- Ada ya Muhula inaweza kulipwa kwa Mkupuo kama jedwali linavyoonesha hapo juu au kwa awamu nne.
- Ada inalipwa mwanzoni mwa Muhula.
**Malipo yote yafanyike kupitia Akaunti A/C No 01J1049102400 CRDB Singida Secondary School**

**<u>TAHADHARI</u>**

Hairuhusiwi kutuma pesa kwa njia ya simu kwa Mwalimu au Mfanyakazi yeyote au kumpatia pesa taslimu, Shule haitahusika na upotevu wa pesa hizo

Malipo ya Ada na Michango yakishalipwa hayatarudishwa kwa yeyote yule

**MICHANGO MINGINE**

| | Maelezo | Muhula wa Kwanza | Muhula wa Pili | Mwaka |
|---|---|---|---|---|
| (a) | Usajili | 30,000 | - | 30,000 |
| (b) | Gharama ya Fomu | 10,000 | - | 10,000 |
| (c) | Ream mbili $A_4$ kwa mwaka (moja kila muhula) | 1 | 1 | 2 |
| (d) | Sare T-Shirt na tai | 30,000 | - | 30,000 |
| (e) | Maabara kidato cha IV | 30,000 | - | 30,000 |
| (f) | Mtihani (NECTA & MOCK) kidato cha IV | 110,000 | - | 110,000 |
| (g) | Mtihani (NECTA) kidato cha II | 40,000 | | 40,000 |

***MICHANGO HII ILIPWE KUPITIA BANK AKAUNTI NA. 01J2049102400 CRDB***

- Viatu vyeusi vya ngozi vya kamba jozi mbili visiwe na maandishi au madoido, soksi ndefu nyeupe jozi mbili kwa wasichana, kwa wavulana soksi za bluu jozi mbili.
- Mahitaji muhimu ya kutumia darasani kama Kalamu ya wino, Penseli, Kifutio, Rula, Vifaa vya Hisabati vya kuchorea (Mathematical set) na kadhalika.
- Daftari za kutosha za (**Counter Book quire 3)** au fedha za kumwezesha kununua daftari kwa ajili ya kuandika wakati wa masomo, shule haitoi daftari.
- Godoro la Sponji lenye upana wa nchi 30 na ni wajibu wako kulitunza godoro, shule haitoi godoro. Pia aje na ndoo ndogo, shuka mbili za rangi ya Bluu Bahari au Pink, blanketi moja, Chandarua ya mbu na sanduku la chuma na vyombo vya kulia chakula ( Bweni).
- Vifaa vya michezo ni muhimu, uje na vifaa vya michezo kama vile, fulana nyeupe ya mikono mifupi, bukta, raba ambazo hazina madoido ya kimaandishi n.k.
- Vifaa vya usafi kwa mwanafunzi wa bweni aje na ufagio wa chelewa pamoja na soft broom au skwiza, kwa mwanafunzi wa kutwa aje na chelewa au soft broom.
- Karatasi za kujaza ambazo zimeambatanishwa na barua hii zijazwe na mzazi au mlezi wako pamoja na picha 2 passport size uziwasilishe shuleni unapofika hapa. Ni jambo muhimu sana kwa mzazi au mlezi kuelewa masharti unayotakiwa kutimiza kabla hujapokelewa shuleni. Fomu hizo zimeambatanishwa kusudi uweze kuzisoma na kuelewa kabla ya kuahidi kuwa utazitekeleza kwa dhati.
- Nguo za nyumbani hazitaruhusiwa shuleni (Bweni).
- Mwanafunzi haruhusiwi Kusuka nywele mtindo wowote ule. Lazima nywele iwe fupi na yakuchana wakati wote.
- Ni marufuku kuja na simu za mkononi. (Mwanafunzi atakayekamatwa na simu atarudishwa nyumbani na hata rudishiwa tena simu)
- Hairuhusiwi kuingiza chakula cha aina yoyote shuleni

1. Shule itafunguliwa rasmi kwa kipindi cha kwanza mnamo tarehe 09/01/2022 (Boarding) na tarehe 10/01/2022 (Day) unatakiwa kufika shuleni siku hiyo au siku mbili kabla ya kufungua shule na mara tu ufikapo ripoti kwa mwalimu wa zamu, zingatia sana tarehe ya kufika shule.

Toa taarifa kwa Mkuu wa Shule haraka endapo unazo sababu za kukubalika za kushindwa kwako kuwahi.

Somo la Computer litafundishwa bure kwa wanafunzi wote.

**MAKOSA YA JUMAA**
**MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULENI NI PAMOJA NA:-**

- Wizi
- Uasherati
- Ulevi wa aina yoyote
- Uvutaji wa bangi/sigara
- Makosa ya jinai
- Kupigana
- Kuharibu kwa makusudi mali za shule
- Kuoa/Kuolewa
- Kutoa mimba
- Kukataa adhabu
- Kumiliki simu au kutumia simu ya mtu mwingine asiye mwalimu.

2. **Mwisho wa Muda wa kuripoti shuleni kwa Wanafunzi wa Bweni ni saa 11:30 Jioni. Tafadhali zingatia hili.**
***Kila mwanafunzi lazima asome sheria hizi kwa uangalifu, azifuate na kuzizingatia. Uvunjaji wa sheria yoyote ya shule hata ikiwa ndogo kiasi gani hautavumiliwa.***

**SHERIA ZA JUMLA**

- Mwanafunzi ni lazima ahudhurie vipindi vyote vinavyomhusu. Ni kosa kubwa kutohudhuria kipindi chochote bila sababu zinazokubalika.

- (a) Yampasa kila mwanafunzi kumpa heshima (kusimama na kumwamkia) wakati wowote mtu anayemzidi umri.
  (b) Kila mwanafunzi lazima awe mtiifu kwa walimu wote, wafanyakazi wote, viranja wa shule na wakuu wengine wote. Ubishi au ujeuri wa aina yoyote kwa walimu au viranja itakuwa ni kosa kubwa.

- Hakuna mwanafunzi anayeruhusiwa kutoka nje ya mpaka wa shule bila cheti kutoka kwa mwalimu wake wa zamu. Mwalimu yeyote au kiranja akimuona mwanafunzi nje ya eneo la shule ana ruhusa ya kuona cheti chake.

- Nguo rasmi za shule (uniform) lazima zivaliwe wakati wote ulivyoelekezwa na shule.

- Mwanafunzi haruhusiwi kwenda nyumbani kwa mwalimu bila sababu maalum. Maeneo waishio wafanyakazi na nje ya mipaka ya shule.

- Kila mwanafunzi lazima aheshimu na kutunza mali ya shule. Ni kosa kuharibu au kutumia vibaya mali ya shule kama vile kuandika ukutani, kuandika katika meza na kadhalika.

- Usafi wa mwili, mavazi, madarasani, viwanja vya shule ni wajibu wa kila mwanafunzi.

- Ni wajibu wa mwanafunzi kuheshimu, kupenda, kuthamini na kufanya kazi kwa uwezo wake wote.
- Kuandika, kupokea na kuwa na picha zenye maneno mabaya ni makosa makubwa. Mwanafunzi haruhusiwi kuandika barua kwa Mkuu yeyote mahali popote bila kupitisha (U.F.S.) kwa Mkuu wa Shule. Aidha jambo lolote litakalofanyika nje ya shule sharti lipate kibali cha Mkuu wa Shule.

- Ruhusa ya kulala nje ya shule itatolewa na Mkuu wa Shule tu kwa kushauriwa na mwalimu mlezi wa bweni.

- Kila mwanafunzi lazima afuate ratiba ya shule kikamilifu.

- **Lugha ya kuzungumza shuleni ni Kiingereza tu.**

**SHERIA YA MADARASANI.**

- Kelele za aina yoyote darasani zinakatazwa, darasani ni mahali pa kujifunzia na si pa kupiga kelele.
- Hakuna mwanafunzi yeyote anayeruhusiwa kuandika ubaoni bila ruhusa.
- Wakati wowote mwalimu akiingia darasani ni lazima wanafunzi wasimame kwa heshima na kumwamkia. Halafu mwalimu atatoa ruhusa ya kukaa.
- Mwanafunzi ambaye atapata wastani wa maksi chini ya 40 atarudia darasa au kufukuzwa kabisa.
- Vyoo vyote lazima vitumiwe vizuri na kuwekwa katika hali ya usafi.
- Ni marufuku kula na kutafuna kitu chochote darasani.

**SHERIA ZA BWENI.**

- Bweni ni mahala pa kulala na si pa kupiga kelele. Usemi wa bwenini uwe na mazungumzo ya maana ya sauti ya chini. Upigaji wa kelele au mayowe ni dalili za ulevi, uhuni hivyo haikubaliki.
- Ni marufuku kwa mwanafunzi yeyote kuchemsha/kupika bwenini, aidha kwa kutumia moto wa kuni, mkaa, mafuta ya taa ama kuunga nyaya za umeme kiolela.
- Usafi wa bweni ndani na nje (Mazingira yanayomzunguka) ni wajibu wa kila mkaaji wa humo.
- Ni makosa kumkaribisha mgeni wa aina yeyote bwenini au katika eneo la bweni.
- Wasichana/Wavulana hairuhusiwi kutembeleana mabwenini.

**SHERIA ZA BWALO NA MAAKULI.**

- Kila mwanafunzi afuate mpango uliowekwa kwa matumizi ya bwalo la maakuli. Ni makosa kumnyima mwanafunzi meza yako ya chakula.
- Utaratibu wa usafi lazima ufuatwe katika ugawaji wa chakula.
- Kila mwanafunzi awe na tabia nzuri mezani, umwagaji ovyo wa chakula hautavumiliwa.
- Usafi wa bwalo na maakuli ndani na nje, ni wajibu wa wanafunzi wote.
- Hakuna mwanafunzi anayeruhusiwa kuingia jikoni bila ruhusa.
- Wizi wa chakula utaadhibiwa kama wizi wa aina yeyote. Na ni makosa kutoa chakula cha shule kwa mtu asiye mwanafunzi bila idhini ya shule.
- Makelele na mayowe wakati wa kula hayatavumiliwa.
- Mwanafunzi haruhusiwi kupeleka chakula bwenini.
- Hairuhusiwi kuingia na ndala, kanga, kofia au vesti ( kaushi) wakati wa chakula.
- Hairuhusiwi kuingiza chakula kisicho kuwa cha shule bwaloni.

**ADHABU.**

- Mwanafunzi yeyote atakayevunja sheria za shule ataadhibiwa mara moja.
- Mwanafunzi anayepewa adhabu ni lazima aifanye kwanza, ubishi au ujeuri wa aina yeyote utaongezewa adhabu hiyo.
- Mwalimu anayo madaraka ya kumuadhibu mwanafunzi atakayevunja sheria hizi au nyingine zozote zitakazotolewa na shule.
- Adhabu ya kumfukuza mwanafunzi shule kwa muda, au kumfukuza kabisa mkosaji itatolewa na Mkuu wa Shule/Bodi ya Shule.
- Adhabu za viranja zitatolewa baada ya kuidhinishwa na Uongozi.

**SARE ZA KUJA NAZO SHULENI**

- Shati mikono mirefu nyeupe
- Suruali ndefu rangi ya kijani nyeusi (wavualana)
- Sketi ndefu chini ya magoti rangi ya kijani nyeusi (wasichana)
- Sketi ndefu ya fundo la mguu (waislamu) hijabu mdomo wa samaki
- Truck suit rangi ya darkblue moja
- Suruali blue nyeusi (wavulana) ya kushindia
- Sketi blue nyeusi (wasichana) ya kushindia

**SHERIA NA ONYO.**

Kila mwanafunzi ni lazima asome na azingatie Sheria za Shule. Kutofanya hivyo ni makosa.

***...................................***
***Benard Ochieng***
***MKUU WA SHULE***
***SINGIDA SECONDARY SCHOOL***

# SHULE YA SEKONDARI SINGIDA

**S.L.P. 589 – SINGIDA**

**SIMU NA: 0759 032918, 0784-716695 & 0679-446992,**

**E-mail: singidasec@gmail.com**

**A/C No 01J1049102400 CRDB**


**FOMU YA KUKUBALI MASHARTI (MZAZI/MLEZI)**

Mimi...................................................................................................mzazi/mlezi wa mwanafunzi................................................................................ nimesoma na kuyaelewa vizuri masharti ya Shule na niko tayari mwanangu asome **Shule hii**.

Mwanangu atakuwa **KUTWA/BWENI** (Kata lisilotakiwa). Na kwamba nitalipa ada na michango yote kama ilivyoainishwa bila usumbufu wowote. Aidha mwanangu atarudia darasa endapo hatafikisha wastani wa **45**.

Naomba Mungu anisaidie katika haya.

Awapo shuleni wafuatao wanaweza kumtembelea

1. .......................................................................... ambayeni.......................................... (taja uhusiano)
2. .......................................................................... ambaye ni ............................................
3. .......................................................................... ambaye ni ............................................
4. .......................................................................... ambaye ni ............................................
5. .......................................................................... ambaye ni ............................................

**Sahihi ya Mzazi/Mlezi: ..............................................** **Tarehe: ..................................................**

**Namba ya Simu ya Mzazi/Mlezi: ..........................................................................................**

**AHADI YA MWANAFUNZI:**

Mimi................................................................................................ (mwanafunzi) nimesoma na kuyaelewa vizuri masharti ya shule na niko tayari kusoma shule hii kwa kuzingatia na kufuata yote. Naahidi kusoma kwa bidii na kutoa ushirikiano kwa **Walimu wangu** ili kutimi

za malengo yangu. Nitajitahidi kuhakikisha napata alama juu ya wastani unaotakiwa. Naamini kwa msaada wa Mwenyezi Mungu na walimu wangu ***NITAWEZA.***

Sahihi ya Mwanafunzi: ................................................ Tarehe: ..................................................

**KUWAONA WANAFUNZI:** *Unaruhusiwa kuja kumsalimia Mwanafunzi kwa kila Jumamosi ya Mwisho wa Mwezi.* Hutaruhusiwa kumwona mtoto wako ukija siku tofauti na hiyo.